**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**-------------**

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/2017 – 2020/2021)

**20 APRILI, 2016**

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Tatu wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuwa na imani kwangu kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo ina jukumu kubwa la kusimamia uchumi na kupanga na kuratibu utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Nitumie fursa hii kuliahidi Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kuwa nitaendelea kutumia uwezo wangu wote, uaminifu na uadilifu ili kuhakikisha kwamba Mpango huu, unasimamiwa vema na kutekelezwa ipasavyo. Nitajitahidi kuhakikisha kuwa rasilimali zitakazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu zinatumika vizuri na kwamba zinasaidia kupunguza umaskini unaowakabili wananchi hususan waishio vijijini.

3. ***Mheshimiwa Spika*****,** napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia**, Mbunge wa Mtwara Vijijini, na Makamu Mwenyekiti **Mhe. Josephat Sinkamba Kandege**, Mbunge wa Kalambo, kwa ushirikiano wao. Maelekezo na ushauri

waliotupatia wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yametusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha Mpango ninaouwasilisha leo.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, **Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji,** Mbunge wa Kondoa, na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, **Dkt. Servacius Beda Likwelile** kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21 ninaowasilisha leo ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 63 (3) (c), ambayo inalitaka Bunge kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango huu wa pili ninaouwasilisha unatokana na ukweli kwamba Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, (2011/12 - 2015/16) unafikia ukomo Juni 2016. Kwa hiyo, Serikali inawajibika kuandaa Mpango mwingine utakaoongoza maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti za kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Mpango unaomaliza muda wake ulijielekeza katika kutanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi na kubainisha maeneo ya kipaumbele kuwa ni

miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu, huduma za fedha, utalii na biashara.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 - 2025/26) wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mpango Elekezi uligawanywa katika mipango mitatu ya miaka mitano mitano, kila mpango ukiwa na dhima mahsusi kuendana na vipaumbele vyake. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utaongoza jitihada za maendeleo kwa kipindi cha kuanzia 2016/17 hadi 2020/21.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia Mpango Elekezi, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulipaswa kujikita katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda. Hata hivyo, mwaka 2015, Serikali ilifanya uamuzi wa kuunganisha mifumo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA katika mfumo mmoja jumuishi ili kuwianisha agenda ya kupunguza umaskini katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Msingi wa uamuzi huo ni kuwa na mfumo mmoja wa utekelezaji wa mipango na hivyo kutanzua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mifumo miwili. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa vipaumbele vingi vinavyofanana na hivyo kutawanya rasilimali za Taifa kidogo kidogo; na kuwepo kwa mfumo dhaifu wa uratibu na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo, uamuzi wa kuunganisha mifumo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA unakusudia kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na

kufanya mabadiliko ya mfumo wa uchumi; kupunguza umaskini; na kuimarisha mfumo wa uratibu, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa. Kufuatia uamuzi huo, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umejumuisha, masuala ya ukuaji na mageuzi ya mfumo wa uchumi na maendeleo ya watu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** utayarishaji wa Mpango umezingatia yafuatayo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango Elekezi wa Miaka 15; mafanikio na changamoto zilizobainishwa katika mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 - 2015/16) na MKUKUTA II; uamuzi wa Serikali wa kufungamanisha na kuwianisha mifumo ya Mpango na MKUKUTA; sera na mikakati mbalimbali ya kisekta, kikanda na kimataifa ambayo Serikali imeridhia, hususan Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs); Dira ya Afrika 2063; Mpango-kazi wa Kuharakisha Maendeleo ya Viwanda Afrika (2008); Sera ya Viwanda ya Afrika Mashariki na mkakati wa utekelezaji wake; Mwelekeo wa Maendeleo ya Viwanda wa SADC (2013 – 2018); na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa SADC (2015 – 2063). Mpango pia umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na hotuba ya Rais ya ufunguzi wa Bunge la 11 iliyoweka msukumo na azma ya kipekee ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kujenga uchumi wa viwanda na kuzipatia ufumbuzi changamoto za msingi kwa maisha ya watanzania, hususan maskini.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya Mpango yalihusisha ushirikishwaji mpana wa wadau, katika hatua zote, kwa lengo la kujenga muafaka wa maeneo ya kipaumbele na mfumo wa utekelezaji. Baadhi ya wadau walioshirikishwa ni pamoja na: Wizara, Idara na Taasisi za Umma; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Asasi za Kiraia; Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti; Washirika wa Maendeleo; na Sekta binafsi. Aidha, Bunge lilishirikishwa kupitia semina ya wabunge iliyofanyika Dodoma, Februari 2016. Aidha, ulifanyika uchambuzi wa kitaalam ulioongozwa na wataalam elekezi (ODI-DFID/REPOA na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango. Pia, maandalizi ya Mpango yaliongozwa na Kamati ya Usimamizi, ambayo wajumbe wake waliteuliwa kuwakilisha makundi mbalimbali wakiwemo sekta binafsi.

## MAPITIO YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA MKUKUTA

### Mwenendo wa Uchumi

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kuwa miongoni mwa nchi zinazokua kiuchumi kwa kasi Barani Afrika. Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7 na kwa miaka mitatu ya mwisho, ukuaji ulizidi kuimarika ukifikia asilimia 7.4 mwaka 2013 na asilimia 7.0 kwa mwaka 2014 na 2015. Wastani wa Pato la kila mtu liliongezeka kutoka shilingi 770,464.3 (sawa na Dola za Marekani 538) mwaka 2010 hadi shilingi

1,997,139.19 (sawa na Dola za Marekani 1,006) mwaka 2015. Ukuaji wa Pato la Taifa, ulichangiwa kwa kiasi kikubwa, na sekta za madini na gesi, ujenzi, uzalishaji na mauzo nje ya nchi ya bidhaa za viwandani, kuimarika kwa huduma za fedha, hali nzuri ya hewa na kuwepo kwa amani na utulivu nchini. Hata hivyo, ukuaji huu bado ni mdogo ukilinganishwa na lengo la wastani wa asilimia 8 au zaidi kwa mwaka. Vile vile, wastani wa Pato la mwananchi lililofikiwa bado ni dogo likilinganishwa na lengo la Dira la kufikia Dola 3,000, ifikapo mwaka 2025.

*Mheshimiwa Spika*, kuhusu mwenendo wa mfumuko wa bei, thamani ya shilingi na hatua zilizofikiwa kupunguza umaskini, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo yangu yaliyoko katika aya ya **12** mpaka aya ya **16** ya kitabu cha hotuba yangu, yanukuliwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge (Hansard).

12. *Mheshimiwa Spika,* mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 19.8 mwaka 2011 na kushuka hadi asilimia 5.6 mwaka 2015, na hivyo kufikia lengo la Mpango la kuwa chini ya asilimia 10. Kiwango cha mitaji ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI) kiliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,813.2 mwaka 2010 hadi Dola za Marekani 2,142 mwaka 2014. Mauzo ya nje pia yaliongezeka kutoka asilimia 16.9 ya Pato la Taifa mwaka 2011 hadi asilimia 23.3 mwaka 2014. Pamoja na mafanikio haya, mfumo wa uzalishaji na mauzo nje umeendelea kutegemea, kwa kiasi kikubwa, mazao-ghafi. Changamoto dhahiri ya mfumo wa uchumi kutegemea mazao-ghafi ni kuyumba mara kwa mara kwa bei katika

soko la dunia, uwezo mdogo wa kutoa ajira, bei duni kutokana na matumizi kidogo ya teknolojia na maarifa katika uzalishaji wake, na pia athari za mabadiliko ya mazingira na tabia-nchi. Haya yote yameishawishi Serikali kuelekeza nguvu zake katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda ili kubadili hali hii.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Kimarekani iliendelea kupungua kutoka wastani wa shilingi 1,566.7 Desemba 2011 hadi shilingi 2,189.1 Februari 2016. Hali hii ni ishara wazi kuwa mahitaji yetu ya fedha za kigeni ni makubwa kuliko mauzo yetu nje. Kwa kiasi kikubwa tumeendelea kununua mahitaji yetu ya msingi kutoka nje ya nchi. Ununuzi kutoka nje uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 3,883.6 mwaka 2011 hadi Dola milioni 4,093.8 mwaka 2015. Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango, akiba ya nchi katika fedha za kigeni imebaki kuwa ya kutosheleza ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa wastani wa miezi minne.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwa na mafanikio ya kutia moyo katika kupunguza umaskini. Tafiti za mapato na matumizi katika kaya, zinaonesha kuwa kiwango cha umaskini mijini na vijijini kimepungua, kuashiria kuwa kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi ya wastani wa asilimia 6.5 iliyofikiwa katika kipindi cha muongo mmoja na nusu uliopita, imeanza kuzaa matunda. Umaskini ulipungua kutoka asilimia 39 mwaka 1992 hadi asilimia 34.4 mwaka 2007, sawa na kupungua kwa asilimia 4.6 kwa kipindi cha miaka 15. Katika kipindi cha miaka 5, kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2012,

umaskini umepungua kufikia asilimia 28.2 mwaka 2012 sawa na asilimia 6.2, na inakisiwa kupungua zaidi hadi asilimia 24.5 mwaka 2015. Hali hii inadhihirishwa na kuzidi kuboreka kwa ubora wa nyumba za makazi, na vyombo vya usafiri, zana na nyenzo za kilimo, na umiliki wa simu za mawasiliano katika kaya.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kiwango hiki cha umaskini, Tanzania ina watu maskini zaidi ya milioni 10, ambayo ni idadi kubwa kuliko baadhi ya nchi Barani Afrika. Idadi hii haishiriki kikamilifu katika juhudi za kuongeza uzalishaji, biashara na mapato ya Serikali. Kwa ujumla umaskini nchini unachochewa na tija na faida ndogo katika sekta ya kilimo ambayo ndiyo mhimili wa watu wengi wanaoishi vijijini. Kwa upande mwingine, hii inachochewa na mabadiliko ya mazingira na tabia-nchi sambamba na kaya nyingi kubeba mzigo mkubwa wa wategemezi kufuatia kasi kubwa ya kuzaliana na athari za magonjwa kama vile UKIMWI. Aidha, ukosefu wa ajira ni moja ya vyanzo vya umaskini na pia ni tishio kwa mustakabali wa amani na utulivu wa nchi yetu. Kati ya vijana 800,000 wanaoingia katika soko la ajira kila mwaka baada ya kumaliza masomo, vijana 200,000 tu ndio wanabahatika kupata ajira katika sekta rasmi.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Taifa yapo katika **Kitabu cha Mpango** (Sura ya Pili).

## Utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2011/12 – 2015/16 na MKUKUTA II unakadiriwa kufikia asilimia 60 ya malengo, ifikapo Juni 2016.

***Mheshimiwa Spika,*** naliomba Bunge lako Tukufu, lipokee maelezo yangu kuhusu mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa na MKUKUTA II kama yalivyo katika kitabu cha hotuba yangu aya ya **18** mpaka aya ya **29** na yasomeke hivyo kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge.

## Miundombinu

18. **Nishati**: uzalishaji wa nishati ya umeme uliongezeka kufikia MW 1,483 mwaka 2014 ikilinganishwa na uwezo wa MW 900 mwaka 2010. Hii ni sawa na asilimia 44.8 ya lengo la MW 2,780 ifikapo Juni 2016. Uunganishaji wa umeme umefikia asilimia 30 (2015) kutoka asilimia 14 mwaka 2010. Ni matarajio ya Serikali kuwa kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam na kufungwa kwa mitambo ya kuzalisha umeme wa kutumia gesi wa Kinyerezi, uzalishaji wa umeme na kasi ya kuunganisha watumiaji vitaongezeka zaidi. Katika eneo la **ujenzi** na ukarabati wa **barabara za lami** lengo lilikuwa ni kuongeza urefu wa km 5,204, ambapo urefu wa km 2,775 ulikuwa umekamilika hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2014. Kwa upande wa **reli ya kati**, lengo lilikuwa ni kukarabati urefu wa km 197 kwa kiwango cha uzito wa ratili 80 kwa yadi

ifikapo Juni 2016, ambapo mpaka sasa km 150 zimekamilika, sawa na asilimia 76.1 ya lengo. Kwa upande wa **usafiri wa anga,** mafanikio ni pamoja na kukamilika kwa hatua ya awali ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe na kukamilika kwa ukarabati wa viwanja vya Arusha, Bukoba, Kigoma, Mafia, Mpanda, na Tabora na kufikia hatua za mwisho za ujenzi wa jengo la abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Mafanikio haya yamesaidia kuongeza idadi ya abiria wa anga kutoka 3,437,608 mwaka 2011 hadi 5,059,739 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 47.2.

19. *Mheshimiwa Spika,* mafanikio mengine yaliyopatikana kwa upande wa miundombinu ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa daraja la Kigamboni – Dar es Salaam na daraja la Jakaya Kikwete katika mto Malagarasi – Kigoma; kuongezeka kwa uwezo wa kuhudumia mizigo **bandarini** kwa asilimia 104 kutoka tani milioni 7.13 mwaka 2011/12 hadi tani milioni 14.6 mwaka 2014/15, na hivyo kuvuka lengo la kufikia tani milioni 9.87; kwa upande wa **TEHAMA,** ujenzi wa mkongo wa Taifa wenye urefu wa km 25,954 umekamilika na kuwezesha mkongo kusambazwa kufikia mikoa 24 na kuunganishwa Zanzibar na nchi jirani, sawa na asilimia 100 ya lengo.

## Kilimo

20. *Mheshimiwa Spika,* mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ukuaji wa sekta ya kilimo kuongezeka kutoka wastani wa asilimia 2.7 kabla ya mwaka 2010 hadi asilimia 3.4 kati ya mwaka 2010 na

2014. Hata hivyo, ukuaji huu bado ni chini ya lengo la Mpango la kufikia asilimia 6 kwa mwaka. Eneo la kilimo cha umwagiliaji liliongezeka kutoka hekta 345,690 mwaka 2010/11 kufikia hekta 461,326 mwaka 2014/15, chini ya lengo la kufikia hekta 1,000,000 ifikapo Juni mwaka 2016. Hata hivyo, mafanikio haya yameiwezesha Tanzania kujitosheleza kwa mahitaji ya nafaka na kuwa na ziada.

**Viwanda**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa ulikuwa wa wastani wa asilimia 7, ukiongezeka kutoka asilimia 6.6 mwaka 2005 hadi asilimia 7.3 mwaka 2014. Ongezeko hili lilichangiwa na uwekezaji mpya na kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya umeme na kuinua matumizi ya uwezo uliopo (capacity utilization). Ongezeko hili ni dogo ikilinganishwa na lengo lililowekwa la kufikia asilimia 12.5 mwaka 2016. Aidha, kwa mujibu wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013, Tanzania ina jumla ya viwanda 50,656, ambapo viwanda vya kati na vikubwa ni 1,769 (asilimia 3.5), viwanda vidogo 48,887 (asilimia 96.5). Mchango wa sekta ya viwanda katika ajira uliongezeka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2010 hadi asilimia 3.1 mwaka 2014.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** imebainika pia kuwa sehemu kubwa ya viwanda vinaendesha shughuli zake katika maeneo yasiyo rasmi, hususan, maeneo ya makazi. Sababu ya viwanda vingi kufanyia kazi katika maeneo yasiyo rasmi ni ukosefu wa mitaa rasmi ya viwanda iliyopimwa na yenye miundombinu, gharama kubwa za

kusajili, wingi wa kodi na ugumu wa kupata ardhi na maeneo ya viwanda. Aidha, miji mingi, na hata mipya, haina maeneo rasmi ya viwanda.

## Maendeleo ya Watu na Huduma za Jamii

23. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio kadhaa katika upatikanaji wa huduma za jamii ni pamoja na: **Elimu** - Kwa upande wa elimu ya msingi - ufaulu uliongezeka kufikia asilimia 57.0 mwaka 2014 kutoka asilimia 53.5 mwaka 2010, elimu ya sekondari, ufaulu umefikia asilimia 69.8 mwaka 2014 kutoka asilimia 50.4 mwaka 2010 na ufaulu kwa kidato cha sita umefikia asilimia 98.3 mwaka 2014 kutoka asilimia 93.8 mwaka 2010. Aidha, kwa upande wa vyuo vya elimu ya juu, udahili uliongezeka kutoka wanafunzi 262,376 mwaka 2010/11 hadi wanafunzi 362,880 mwaka 2013/14. Kwa upande wa **afya,** vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua na kufikia vifo 54 mwaka 2013 kutoka 81 mwaka 2010 kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa, vifo vya akina mama wajawazito vimepungua kutoka 454 mwaka 2010 hadi vifo 432 mwaka 2013 kati ya vizazi hai 100,000, chini ya lengo la kufikia vifo visivyozidi 265 mwaka 2015. Kwa upande wa upatikanaji wa **huduma za maji** safi vijijini, huduma imewafikia wananchi 20,957,855 sawa na asilimia 72.

## Huduma za Fedha, Biashara na Utalii

24. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo yalikuwa ni kuimarisha mitaji ya benki za umma za maendeleo za TIB na TADB kwa kuongeza kiasi cha shilingi bilioni 500 kwa kila moja. Malengo haya

hayakufikiwa, mtaji wa TIB uliongezwa kufikia bilioni 212 na TADB mtaji wa shilingi bilioni 60 tu. Kwa upande wa **biashara,** mchango wa Tanzania katika biashara ya dunia uliongezeka kutoka asilimia 0.04 mwaka 2010 hadi asilimia 0.048 mwaka 2014 ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 0.1. Katika sekta ya **utalii,** Tanzania imeendelea kufanya vizuri. Watalii kutoka nje waliongezeka kutoka 784,709 mwaka 2010 hadi 1,142,217 mwaka 2014 na mapato yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 1,254.5 kufikia dola milioni 2,006.32 kwa mtiririko huo. Kwa upande wa uboreshaji wa **mazingira ya biashara**, Tanzania imekuwa ikipoteza uwezo wake wa kushindana kibiashara na kuvutia uwekezaji. Kwa mfano, Tanzania ilishika nafasi ya 126 (2010), 134 (2014), 140 (2015) na inatarajiwa kushika nafasi ya 139 (2016) kati ya nchi 186 (kwa vigezo vya Benki ya Dunia). Kigezo hiki ni muhimu katika kubainisha uwezo wa nchi kushindana kibiashara na kuvutia uwekezaji.

**Ushiriki wa Sekta Binafsi**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango umezidi kuimarika mwaka hadi mwaka. Kwa ujumla, kumekuwa na ongezeko la mitaji ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje kutoka dola za Marekani milioni 1,813.2 mwaka 2010 hadi milioni 2,142.0 mwaka 2014. Vile vile, uhawilishaji wa fedha (remittance) binafsi kutoka nje uliongezeka kutoka asilimia 0.13 hadi 0.22 ya Pato la Taifa. Mtaji wa sekta binafsi uliongezeka kutoka shilingi bilioni 7,570.2 mwaka 2010 hadi bilioni 12,861.1 mwaka 2013, hususan kutokana na ujenzi wa

miradi mikubwa ya viwanda vya saruji na vifaa vya ujenzi, nyuzi na nguo, na bidhaa za chakula.

**Utawala Bora na Uwajibikaji**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kuwa moja ya nchi chache Barani Afrika zenye utulivu wa kijamii na kisiasa. Hii ni kielelezo kuwa kuna utawala thabiti. Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea na juhudi za kujenga uwezo wa utoaji wa huduma na usimamizi wa sheria na utoaji wa haki, mapambano dhidi ya rushwa, na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na mali za umma.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na MKUKUTA II yapo katika **Kitabu cha Mpango** (Sura ya Pili).

**Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Hatua Zilizochukuliwa**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango ni pamoja na: upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi; ushiriki mdogo wa sekta binafsi; baadhi ya miradi ya kibiashara kuendelea kubaki katika bajeti ya Serikali na hivyo kudumaza uwekezaji wa sekta binafsi; upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji ikiwemo viwanda; matayarisho hafifu ya miradi ikiwa ni pamoja na mapungufu makubwa ya maandiko ya miradi, ripoti za uchambuzi yakinifu wa mahitaji ya fedha, upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kimazingira; vipaumbele vingi; na mazingira duni ya kufanya biashara.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hizi ikiwemo: kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha, hususan fedha za miradi ya Matokeo Makubwa Sasa na miradi ya Kitaifa ya Kimkakati; kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuchochea uwekezaji wa Sekta Binafsi, hususan katika viwanda; na kuendelea kuimarisha upatikanaji wa miundombinu wezeshi katika maeneo ya miradi ya maendeleo. Hatua nyingine ni kuandikwa kwa mwongozo wa usimamizi wa miradi na kutoa ufafanuzi juu ya matumizi ya mwongozo huo. Aidha, hatua zinaendelea kuchukuliwa kuboresha mfumo wa upatikanaji wa takwimu, kuimarisha upatikanaji wa ardhi kwa kutenga fedha kwa ajili ya fidia katika maeneo ya uwekezaji.

## MPANGO WA PILI WA MANDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21 una dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Kiuchumi na Maendeleo ya Watu – *Nurturing Industrialisation for Economic Transformation and Human Development".* Msukumo wa Mpango huu ni kuhakikisha kuwa rasilimali na fursa za nchi zinatumika vizuri katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na uwezo wa kupunguza umaskini.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** msisitizo katika maendeleo ya viwanda nchini siyo jambo jipya. Tangu Uhuru maendeleo ya viwanda yamekuwa yakipewa kipaumbele katika mipango ya vipindi mbalimbali, japo utekelezaji wake umekuwa ukitumia mikakati inayotofautiana kwa kuzingatia mfumo wa sera za usimamizi wa uchumi. Kabla ya Azimio la Arusha, sekta ya viwanda iliendelezwa na sekta binafsi na Serikali. Baada ya Azimio la Arusha, Serikali ilitekeleza siasa ya ujamaa na kujitegemea ambapo shughuli zote kuu za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na viwanda zilianza kumilikiwa na kuendeshwa na Serikali. Aidha, msisitizo ulikuwa kujitegemea ambapo viwanda vililenga kuzalisha bidhaa zinazotumika kwa wingi nchini na hivyo kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje (import substitution). Viwanda vichache vilijikita katika kuchakata mazao ya kilimo kwa ajili ya kuuza nje. Ili kuhakikisha viwanda na soko la ndani vinalindwa, sera ya kudhibiti biashara iliwekwa. Kuyumba kwa uchumi nchini na kuvunjika kwa mfumo wa kisoshalisti duniani kuliifanya Tanzania kuachana na mfumo wa uchumi wa ujamaa na kujitegemea na badala yake kufungulia milango kwa wawekezaji binafsi na kuondoa vikwazo vya biashara na uwekezaji.

**Hali ya Viwanda**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** tangu kuanza kwa ubinafsishaji wa mashirika ya umma mwaka 1992, viwanda 106 vimebinafsishwa kwa wawekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi. Lengo lilikuwa ni kuongeza ufanisi wa usimamizi, uzalishaji, ajira, kupunguza uagizaji wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa hapa nchini na kuongeza mauzo

ya bidhaa nje ya nchi. Kati ya viwanda vilivyobinafsishwa, viwanda 34 vinaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Viwanda 33 vinaendeshwa kwa hasara na viwanda 39 vya bidhaa mbalimbali kama vile ngozi, chuma, korosho, zana za kilimo, sabuni na mafuta ya kupika vimefungwa kabisa kutokana na changamoto za kiutendaji, mitaji, teknolojia, nishati, malighafi au kutokuzingatiwa kwa mikataba ya mauzo. Hatua za uchambuzi kwa lengo la kubainisha mfumo wa kuvifufua viwanda vilivyobinafsishwa zimeanza na zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango (2016/17).

33. *Mheshimiwa Spika,* uendelezaji wa viwanda nchini ni jambo la kutiliwa mkazo katika mipango yetu ijayo ili kutuwezesha kufikia azma ya kuwa miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025. Maendeleo ya viwanda yanashikilia ufunguo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kutokana na uwezo wake wa kutengeneza ajira nyingi zenye faida na kuchochea maendeleo ya teknolojia. Mifano kutoka nchi mbalimbali inabainisha kuwa maendeleo ya viwanda ndio msingi na chimbuko la ustawi wa nchi hizo kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.

34. *Mheshimiwa Spika,* katika Mpango huu, uzoefu wa nchi mbalimbali umetumika katika kubainisha mwelekeo wa ujenzi wa viwanda nchini. Uzoefu huo unabainisha kuwa: Serikali ina wajibu mkubwa katika hatua za awali za ujenzi wa uchumi wa viwanda hususan katika kuweka mazingira mazuri ya kibiashara; kuweka

mfumo mzuri wa kibenki, ikiwa ni pamoja na kuanzisha benki maalum za maendeleo za kisekta kusaidia upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na kwa gharama nafuu, na kuainisha sera na taratibu dhahiri za kuchochea maendeleo ya sekta binafsi, uhawilishaji teknolojia na ukuzaji wa fani za kitaalam zinazotakiwa katika maeneo ya kipaumbele.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itatumia taasisi zake za kibiashara kama mkakati wa kuingia ubia na sekta binafsi katika kuvutia viwanda vyenye maslahi makubwa kitaifa, kibiashara, kiteknolojia au kuzalisha bidhaa muhimu kwa soko la ndani; kusaidia sekta binafsi ya ndani kuingia na kujiimarisha katika shughuli za viwanda hususan viwanda mkakati na shughuli nyingine muhimu; na kuwianisha sera za viwanda, biashara, elimu, ufundi, tafiti na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Miongoni mwa masuala yatakayopewa kipaumbele katika bajeti ni utafiti na ubunifu na pia maendeleo ya miji na uendelezaji wa maeneo ya biashara kubwa na ndogo. Halmashauri za Miji na Wilaya na miji midogo ina wajibu wa msingi wa kulea maendeleo ya viwanda na biashara katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kulinda maendeleo ya viwanda mkakati.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu uzoefu wa nchi zingine yapo katika **Kitabu cha Mpango** (Sura ya Tatu).

**Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango wa Pili**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango una maeneo makuu manne ya kipaumbele, ambayo ni;

**(i)** **Kukuza Uchumi na Kujenga Msingi wa Uchumi wa Viwanda:** Eneo hili linahusisha hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika sekta za uzalishaji, ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo, viwanda, madini na utalii. Vigezo vya uteuzi wa miradi ya kundi hili ni pamoja na (i) uwepo wa fursa za kipekee za rasilimali za uzalishaji na masoko ya bidhaa (ii) uwezo wa bidhaa hizo, kushindana au kuhimili ushindani wa kibiashara; (iii) bidhaa zenye kutumika kwa wingi katika soko la ndani; (iv) uzalishaji wa bidhaa zinazotumia teknolojia inayoendana na uwezo wa nchi na rasilimali zinazopatikana kwa wingi na nafuu; (v) Miradi itakayowezesha Tanzania kutumia vizuri zaidi fursa yake ya kijiografia kama mhimili wa biashara ya usafirishaji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati; na (vi) Uendelevu wa ukuaji na mabadiliko ya uchumi baada ya Mpango.

**(ii)** **Kufungamanisha Maendeleo ya Uchumi na Maendeleo ya Watu:** Hii itahusisha kupanua fursa za upatikanaji wa elimu (kuanzia malezi na elimu ya awali, elimu bora kwa wote, na fursa za kujiendeleza kitaaluma na ujuzi) kumwezesha mtu kujiajiri au kuajiriwa, kuimarisha na kuboresha afya ya mwananchi kama vile huduma za

matibabu, usalama wa chakula na upatikanaji wa viini lishe vya mwili (nutrition), maji safi, mazingira safi ya kuishi na hifadhi ya jamii.

(iii) **Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji:** Mpango unalenga kuimarisha mifumo ya kisheria ili iwe rafiki katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje pamoja na kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za msingi kwa uwekezaji, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nishati ya umeme, miundombinu ya reli, barabara, bandari, usafiri wa anga, usafiri wa majini, maji na TEHAMA.

(iv) **Kuimarisha Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango:** Maeneo mahsusi ni kutanzua vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya Mpango. Aidha, eneo hili limeainisha marekebisho yanayopaswa kufanyika ya kisera, sheria na taratibu za kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Mpango.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya miradi imepewa sifa kuwa miradi ya kielelezo (flagship projects). Miradi hii ni ile mikubwa na ambayo matokeo yake yanatarajiwa kusukuma au kuwezesha ufanisi wa utekelezaji na uwekezaji wa miradi mingine. Miradi hii ni: Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma; Mradi wa Chuma Liganga; Maeneo Maalum ya Uwekezaji; Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini; Ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake kwa Kiwango cha

*Standard Gauge*; Mji wa Kilimo - Mkulazi; Ufufuaji wa Shirika la Taifa la Ndege; na Kusomesha vijana wengi katika fani na ufundi stadi unaohitajika katika maeneo ya kipaumbele. Miradi hii imefungamanishwa na miradi mingine ya kimkakati katika mfumo wa maendeleo au maeneo maalum ya uchumi.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu maeneo ya kipaumbele ya Mpango yapo katika **Kitabu cha Mpango** (Sura ya Nne).

## Ugharamiaji wa Mpango

40. ***Mheshimiwa Spika,*** shilingi trilioni 107 zitahitajika kugharamia utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, sawa na wastani wa shilingi trilioni 21.4 kila mwaka. Kati ya fedha hizo, Serikali itachangia shilingi trilion 59, sawa na trilioni 11.8 kila mwaka. Kama ilivyojidhihirisha, kuna ongezeko kubwa la fedha zinazohitajika kugharamia Mpango wa Pili ikilinganishwa na ule wa Kwanza. Hii imesababishwa na kuzingatia uzoefu tulioupata katika utekelezaji wa Mpango wa kwanza na pia ukubwa wa miradi tarajiwa, sambamba na nia ya kuchochea upatikanaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** uzoefu wa nchi nyingine unabainisha kuwa mkakati wa ujenzi wa viwanda aghalabu huvutia misaada kutoka nje. Mantiki yake ni kuwa nchi haina budi kuwa na mkakati

mahsusi wa kukusanya fedha kuwezesha utekelezaji wa Mpango kwa ufanisi. Mpango unaainisha maeneo mawili ya vyanzo vya fedha, yaani, mapato ya Serikali yakihusisha mapato ya kodi na yasiyokuwa ya kodi, mikopo na misaada kutoka nje. Eneo la pili ni sekta binafsi ya ndani na nje. Ni jambo lililo bayana kuwa, kwa kiasi kikubwa, utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo utategemea ushiriki wa Sekta Binafsi. Kuwezesha Sekta binafsi kuwekeza katika miradi ya maendeleo, Serikali imeweka mikakati ya kujenga na kuboresha miundombinu wezeshi (nishati ya umeme, reli, barabara, bandari, usafiri wa anga na majini); kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuhamasisha na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma. Fedha za Serikali zitatumika kama chambo kuvutia ushiriki wa sekta binafsi.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyokwisha eleza, Mpango huu unabainisha miradi mikubwa ya kielelezo. Naomba nisisitize kuwa miradi hii itatekelezwa kwa kiwango kikubwa na sekta binafsi moja kwa moja au kwa ubia na sekta ya umma.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu ugharamiaji wa mpango yapo katika **Kitabu cha Mpango** (Sura ya Tano).

## Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Pili utatekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka. Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa kila mwaka utaelekeza utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kurejea hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika na kubaini mahitaji ya rasilimali. Wizara na Taasisi nazo zitafanya mapitio ya mikakati ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mpango huu. Kusudi la uchambuzi huu ni kuhakikisha vipaumbele vya Mpango huu vinazingatiwa katika miaka yote mitano ya utekelezaji wake.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu mikakati ya utekelezaji wa mpango huu yapo katika **Kitabu cha Mpango** (Sura ya Sita).

## Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha na Mipango itakuwa na wajibu wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21 na kutoa taarifa katika ngazi zote stahiki na kwa wakati. Sura ya sita ya kitabu cha Mpango imeainisha viashiria na malengo mahususi kwa ajili ya kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara na Taasisi za Umma zinazohusika moja kwa moja katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo nazo zitawajibika kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo  katika maeneo yao na kuandaa taarifa za utekelezaji kulingana na miongozo itakayotolewa na Serikali. Tathmini ya kina ya utekelezaji wa Mpango katika kipindi cha kati na mwisho vitafanyika kwa kuwatumia watathmini wa kujitegemea, nje ya mfumo wa Serikali, ili kuwa wa wazi na huru zaidi. Aidha, tathmini hiyo itazingatia vigezo na malengo yaliyoainishwa katika maeneo mbalimbali ya Mpango.  Wasimamizi wakuu wa miradi watakao thibitika kushindwa kufikia malengo ya Mpango wawajibike wenyewe au wawajibishwe.

**Malengo ya Mpango**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya malengo ya Mpango huu ni pamoja na yafuatayo:

(i) Kasi ya ukuaji wa uchumi kuongezeka kutoka asilimia 7.0 mwaka 2015 hadi asilimia 10 mwaka 2020;

(ii) Pato la wastani kwa kila mwananchi kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani 1,006 mwaka 2015 hadi 1,500 mwaka 2020;

(iii) Uwekezaji wa moja kwa moja nchini (FDI) kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.14 mwaka 2014 hadi Dolaza Kimarekani bilioni 5 mwaka 2020;

(iv) Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na kodi kutoka asilimia 12.1 ya Pato la Taifa mwaka 2014/15 hadi asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21.

(v) Umaskini wa mahitaji ya msingi kupungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 16.7 mwaka 2020/21;

(vi) Idadi ya wahitimu kutoka Vyuo vya Ufundi Stadi (VET) kuongezeka kutoka 150,000 (2014/15) hadi 700,000 (2020/21);

(vii) Vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano kupungua kutoka 81 mwaka 2014/15 hadi 45 mwaka 2020/21 kwa kila vizazi hai 1000;

(viii) Vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kupungua kutoka 432 kwa 2014/15 hadi 250 mwaka 2020/21 kwa kila vizazi hai 100,000;

(ix) Huduma ya maji safi na salama kwa maeneo ya vijijini kuongezeka kutoka asilimia 67 mwaka 2014/15 hadi asilimia 80 mwaka 2020/21;

(x) Uzalishaji wa umeme kuongezeka kutoka MW 1,501 mwaka 2015 hadi MW 4,915 mwaka 2020 na Usambazaji wa umeme kufikia asilimia 60 ya Watanzania (2020) ikilinganishwa na asilimia 36 hivi sasa;

(xi) Kuongeza mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi kutoka asilimia 24 (2014) hadi asilimia 30 (2020) ya mauzo yote nje ya nchi;

(xii) Kujitosheleza katika utengenezaji wa sare na viatu kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na katika vyombo vya ulinzi na usalama; na

(xiii) Idadi ya Watalii kuongezeka kutoka 1,140,156 (2014) hadi 2,000,000 (2020) na mapato yatokanayo na utalii kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2 (2014) hadi Dola za Kimarekani bilioni 3.6 (2020).

Hatua za kimkakati za kuendeleza viwanda nchini na malengo yameelezwa kwa kirefu katika **Sura ya Nne** ya kitabu cha Mpango.

## Matokeo ya Utekelezaji

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango utawezesha ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda na kuimarisha jitihada za kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa kipato. Pia, ustawi wa jamii ya Watanzania utakuwa bora zaidi kutokana na kuongezeka kwa fursa za ajira na biashara kufuatia kuongezeka kwa viwanda nchini. Kwa ujumla, matokeo ya utekelezaji wa Mpango ni pamoja na: kuimarika kwa kasi na ukuaji mpana wa uchumi kwa manufaa ya wananchi walio wengi ambapo uchumi unatarajiwa kukua kutoka asilimia 7.0 mwaka 2015 hadi asilimia 10 mwaka 2020; kuongeza kasi ya

kupunguza umaskini ambapo Pato la wastani kwa kila mwananchi litaongezeka kutoka Dola za Kimarekani 1,006 mwaka 2015 hadi 1,500 mwaka 2020; kuongeza fursa za ajira kwa wote, hususan vijana na akina mama; kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma za jamii; kubadili mfumo wa biashara kwa kuongeza mauzo nje ya bidhaa za viwandani badala ya kuuza bidhaa ghafi na wakati huo huo kulinda hifadhi ya mazingira.

## HITIMISHO

50. ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 9 Desemba, 2016 tutaadhimisha miaka 55 ya Uhuru wa nchi yetu. Maana yake ni kuwa, kiumri nchi yetu si changa tena. Ni nchi yenye umri wa mtu mzima anayepaswa kuwa na familia yake na uwezo wa kujitegemea kimaisha na kiuchumi. Hivyo basi, kama nchi, hatupaswi kuwa wategemezi! Sharti tujitegemee. Katika hili hakuna njia ya mkato. Tunapaswa kujidhatiti kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kutoka katika vyanzo vyetu vya ndani kwa nguvu zote. Aidha, matumizi ya starehe, ambayo katika hali halisi ya maisha, uchumi wetu na mantiki nzima ya kutaka kuondokana na umaskini na utegemezi wa kibajeti, hatuna budi kuondokana nayo.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** kuna masuala ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuondokana nayo kwa vile yanatubebesha mzigo mzito sisi sote kama Taifa, lakini hususan wale walio maskini na wanyonge zaidi katika jamii. Kazi hii siyo rahisi. Ni vita inayohitaji mageuzi ya mfumo wa maisha kwa kuukana kwa dhati utamaduni wa kuishi maisha kwa kipato

tusichokimudu au tunachokipata visivyo halali au bila kufanya kazi ipasavyo. Tunajua baadhi ya watu, hasa wale wachache waliokuwa wananufaika zaidi na mfumo huo, mageuzi haya yatawauma na watajaribu kuyapinga. Ndiyo sababu Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, amekuja na kauli ya "Kutumbua Majipu". Wote tunafahamu kuwa kutumbuliwa jipu kunaambatana na maumivu makali lakini hii ndiyo njia pekee ya kupona.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nisisitize kuwa Serikali ya Awamu ya Tano haitaona huruma wala kuchoka katika kutoa tiba hii kwa wahusika wote katika jamii yetu. Watu wachache wanaonenepa juu ya migongo ya masikini lazima watumbuliwe. Hakuna kurudi nyuma. Habari ya mjini ni **mbele kwa mbele**! Huruma yetu na wajibu wetu mkubwa ni kwa wachapa kazi na masikini wa nchi yetu ambao wameendelea kuteseka kwa miaka mingi kwa kukosa malipo stahili kwa jasho lao na hata kukosa mahitaji ya msingi na huduma bora.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** uchumi wa viwanda ndiyo njia ya uhakika katika kufikia Maendeleo Endelevu iliyotumiwa na nchi nyingi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi duniani. Kama wenzetu wanatokea hapo, basi ni busara pia kwetu kupitia njia hiyo hiyo lakini kwa kutumia vizuri fursa tulizo nazo hapa nchini na zinazochomoza Kikanda na Kimataifa na vile vile kujiandaa kukabiliana na vihatarishi vilivyoko mbele yetu. Tumeamua kujipanga upya kujenga uchumi wa viwanda. Lakini lililo dhahiri katika njia hii ni kuwa kutakuwa na vikwazo, ikiwa ni pamoja na

ushindani mkali katika masoko ya mitaji na bidhaa. Ili tuvuke tunahitaji dhamira ya dhati ya kuibadilisha nchi yetu kuwa sehemu bora zaidi ya kuishi kwa wananchi wetu wote. Kubwa kwetu ni kushikamana na kuamini katika njia tuliyoichagua kupita. Nawaomba Watanzania wenzangu tushirikiane ili tumsaidie Rais wetu kutuongoza na kutuvusha kufikia azma yetu ya kujenga uchumi wa viwanda, wenye kutoa ajira na ujira mzuri na hatimaye kila mmoja wetu aweze kufaidi matunda ya uhuru wetu.

54. ***Mheshimiwa Spika***, kufanya kazi kwa bidii, nidhamu ya hali ya juu, maarifa, uadilifu, kutumia teknolojia na ubunifu na kuzingatia Sheria na Taratibu za nchi ili kudumisha amani yetu ndiyo misingi itakayotuvusha kutoka hapa tulipo sasa. Kila Mtanzania ni la zima ajitoe kutumikia nchi yake na watu wake. Mimi naamini kabisa kuwa tukifanya haya, chini ya Uongozi shupavu na uthubutu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Jemedari wetu, huu ndio utakuwa mwanzo wa Tanzania mpya ambayo wote tunaitamani. Tanzania yenye neema, Tanzania shindani, ambayo itakuwa nguvu kuu ya kiuchumi (Economic Power House) katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kwa unyenyekevu, nimalize hotuba yangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na kitabu cha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 inapatikana katika tovuti za Wizara ya Fedha na Mipango ***www.mof.go.tz*** na ***www.mipango.go.tz***

56. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

**Mungu ibariki safari yetu ya "HAPA KAZI TU" ya kuijenga Tanzania mpya.**

57. *Mheshimiwa Spika,* naomba kutoa hoja.